Nuru ya Kiswahili, Juzuu 1(2), Desemba 2022: 164 - 183

# Utumizi wa Mbinu za Fasihi Simulizi katika Nyimbo za Injili: Mfano kutoka Wimbo wa Bahati Bukuku Uitwao "Kampeni"

**John P. Madoshi**
**Mhadhiri, Chuo Kikuu cha Dodoma**

doshijope@yahoo.com

**Ikisiri**

Makala hii imeangalia kwa kina utumizi wa mbinu za fasihi simulizi ya Kiswahili katika nyimbo za injili kwa kutumia wimbo uitwao 'Kampeni' wa Bahati Bukuku uliohifadhiwa katika picha jongefu. Nadharia ya uhakiki wa kimtindo imetumika kufafanua matini katika uchambuzi wa kazi hii ya fasihi. Katika wimbo huu, mbinu mbalimbali za fasihi simulizi zimetumika kuijenga kazi hii. Kupitia picha jongefu, mhusika mkuu anatumia njia ya majigambo, chuku na kejeli ambavyo ni nduni za fasihi simulizi. Wimbo huu pia unatawaliwa na usimulizi. Usimulizi huu wa kifasihi ingawa umekusudiwa kutoa mafundisho, umechota kwa sehemu kubwa sifa anuai za fasihi simulizi na kuziingiza katika matumizi ya injili. Katika wimbo huu pia, kuna mandhari mbalimbali zilizotumika kibunilizi kama vile: mandhari ya duniani, Jehanamu na mbinguni. Fanani katika wimbo huu anaruhusu wahusika watokee kama vionwa katika picha hiyo jongefu lakini maneno yote yasemwe na yeye msimuliaji. Wimbo huu unaonesha kuwa fasihi simulizi inaouwezo wa kubadili uwasilishwaji wake na kuifanya ikidhi matakwa mbalimbali ya jamii. Kupitia wimbo huu ni bayana kuwa fasihi simulizi inakubali mabadiliko na kuifanya iingie katika nyanja anuai kama katika picha jongefu za muziki wa injili.

**Dhana za Msingi:** Fasihi simulizi, picha jongefu, muziki wa injili, motifu, majigambo

## Utangulizi

Wataalamu mbalimbali wanaitazama fasihi simulizi kama kazi ya sanaa inayotungwa na mtu kichwani na kupelekwa mbele ya hadhira kupitia njia ya mdomo na vitendo bila kuhusisha maandishi (Mulokozi, 1996). Fasihi simulizi hurithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine kwa njia ya mdomo kupitia namna mbalimbali kama vile: vitendawili, hadithi nyimbo na ngoma. Uwasilishaji wa fasihi simulizi hutegemea kwa kiasi kikubwa sauti na vitendo ikihusisha sanaa (Wanjala, 2011). Hata hivyo, kutokana na maendeleo makubwa ya tehama, fasihi simulizi leo inaweza kuhifadhiwa katika vyombo kama redio, runinga, video na intaneti na kusambazwa na msanii kwa mdomo ama sauti na picha kupitia vyombo vya mawasiliano (Mutembei, 2006:11). Kwa ufupi fasihi simulizi ni sanaa ambayo hutegemea fanani afikishe ujumbe wake kwa hadhira kibunifu kwa njia mbalimbali. Katika makala hii, tutajadili wimbo wa injili wa Bahati Bukuku uitwao "Kampeni" ambao umeimbwa kupitia picha jongefu ukitumia mbinu mbalimbali za fasihi simulizi.

Wimbo wa Bahati Bukuku wenye mhusika mkuu aitwaye Tupatupa umeathiriwa na masimulizi kiasi cha kumfanya mtu ausikiaye ajiulize nini hasa yalikuwa makusudi ya mtunzi wa wimbo huu. Kupitia picha jongefu mtazamaji anaweza kuona kuwa mwimbaji amejivika libasi zenye kufanana na msimuliaji katika ngano akiwa amekusanya hadhira hai inayomsikiliza wakati anasimulia. Pengine upekee wa wimbo huu uko katika hadhira na wahusika ambao hawapewi nafasi ya kusema ila mtambaji pekee ndiye hubaki akisimulia. Mbinu hii kwa hakika ni mbinu ya fasihi simulizi ambamo mtambaji hujivika uhusika akichukua nafasi ya kila mhusika na kuwa msemaji wa wahusika wote. Hali hii inajitokeza katika wimbo huu ambamo msimuliaji anaruhusu wahusika watokee kama vionwa tu lakini

maneno yote yasemwe na yeye msimuliaji. Katika makala hii tutaangalia sehemu ambazo mbinu hii ya usimuliaji imetamalaki na dhima ya masimulizi haya ambayo kwa hakika ni ya kifasihi simulizi lakini yameingizwa katika uimbaji wa nyimbo za injili.

**Nadharia ya Utafiti**

Nadharia ya uhakiki wa kimtindo imetumika kufafanua matini katika uchambuzi wa kazi hii ya fasihi. Nadharia hii kulingana na Barry (2002) ilianza kama nadharia wakati wa urasmi mkongwe. Ilitumiwa na wachambuzi kama vile Aristotle na Cicero katika enzi ya Uyunani na Rumi ya kale. Awali nadharia hii ilijihusisha na masimulizi, uteuzi wa maneno na mpangilio wa namna ya kuunda ruwaza. Mwishoni mwa miaka ya sitini na mwanzoni mwa miaka ya sabini, nadharia hii ilipata nguvu kwa kuibuka kwa wanazuoni walioona vyema kuiendeleza. Hawa ni pamoja na Catman (1967), Leach (1969) na Hilary (1973). Hata hivyo nadharia hii ilitumika kwa ufinyu kwani wasomi hawa walijikita kutazama vipengele vya ki-isimu. Nadharia hii hatimaye iliingia katika nyanja ya fasihi mnamo miaka ya themanini baada ya Leech na Short (1981) kuiona kuwa ilifaa kutumiwa kuangalia mtindo wa lugha katika muktadha kwa lengo fulani. Simpson (2004) anaona kuwa nadharia hii inaweza kutumika kuchunguza mitindo ihusishayo uteuzi wa maneno katika sarufi, usimulizi, itikadi, muwala na mshikamano wa mtindo. Aidha anaona kuwa nadharia hii inaweza kutumika katika mazungumzo na mbinu za uwasilishaji wa usemi na mawazo na mambo kadhaa yahusuyo mtindo katika matini lugha. Kwa uchambuzi wa matini katika makala hii, nadharia hii imetumika kwa kuzingatia mandhari, uhusika, dhima ya utambaji na motifu ya safari ambamo maingiliano ya kimtindo yamejitokeza.

**Matokeo ya Utafiti**

Utafiti umeonesha kuwa wimbo wa "Kampeni" umetumia mbinu mbalimbali za fasihi simulizi kama vile kujivika ufanani, kauli mbalimbali za usimulizi, majigambo, na motifu ya safari. Kabla ya kuwasilisha matokeo, ufafanuzi kuhusu wimbo huo umetolewa.

**Ufafanuzi kuhusu wimbo wa Bahati Bukuku "Kampeni"**

"Kampeni" ni wimbo uliotungwa na mwimbaji wa nyimbo za injili aitwaye Bahati Bukuku. Wimbo huu umerekodiwa na kuhifadhiwa kupitia sauti na picha jongefu. Mhusika mkuu katika wimbo huu anaitwa Tupatupa. Tupatupa anaelezwa katika wimbo huu kuwa mtu aliyependa anasa za ulevi na zinaa. Siku moja baada ya kulewa, Tupatupa anapata ajali na kupoteza fahamu. Akiwa hajitambui, anatokea malaika na kumuuliza anachagua kwenda wapi kati ya mbinguni ama Jehanamu. Tupatupa anachagua kwenda mbinguni. Malaika anamweleza kuwa hana budi kupelekwa sehemu zote ili afanye uchaguzi sahihi. Tupatupa anapelekwa Jehanamu kwanza. Anafurahishwa na starehe na ukarimu anaooneshwa kule Jehanamu.

Anapopelekwa mbinguni, hafurahishwi na maisha ya kule yenye kutawaliwa na ibada muda wote. Kwa hiyari yake mwenyewe, Tupatupa anaomba arejeshwe Jehanamu. Anapofika Jehanamu, haoni starehe alizoziona awali ila mateso kwa waovu. Tupatupa anasihi arejeshwe tena mbinguni badala ya kubaki kwenye mateso ya Jehanamu. Malaika anamwambia hakuna uwezekano kwani mlango wa rehema umefungwa.

**Mbinu ya usimuliaji katika Wimbo wa Bahati Bukuku; "Kampeni"**

Ukitazamwa kupitia picha jongefu, mtambaji anaanza kwa kipande kifupi cha wimbo akiieleza hadhira makusudi ya usimulizi huu. Katika kipande cha wimbo kilicho katika utangulizi, msimuliaji anamtaja mhusika mkuu

katika kisa hiki kuwa jina lake aliitwa Tupatupa. Aidha msimuliaji anabainisha wasifu wa nje wa mhusika huyu kuwa alikuwa temedeni na mwenye kujawa ukwasi. Mwandishi anataka tufahamu kuwa sifa hizi mbili kuu zinamfanya awe ashiki ya kila mtu kutengeneza ukuruba naye kwa lengo la kuvutia neema ya mapato kutoka kwa mkwasi huyu kama tunavyoweza kuona katika mishororo ifuatayo:

> Alikuwapo baba jina lake Tupatupa,
> Ebu ngoja leo tulia nikwambie.
>
> Alikuwa tajiri tena mwenye sura nzuri
> Kila aliyemwona alijua mambo sawa.
>
> Mzee Tupatupa alipoona wadada
> Kila aliyemwona alijua amepona
>
> Mambo yake yalikuwa ni hivi
> Ebu ngoja leo sikia nikwambie.

Msimuliaji anabainisha udhaifu wa mhusika huyu kuwa alipenda uasherati kwani alipoona wasichana wazuri alijua atawapata ili aweze kuhusiana nao katika anasa na mapenzi. Mwanzo huu pekee unatosha kuonesha lengo la simulizi hii kuwa mwimbaji anakusudia kufundisha somo la maadili ya dini kupitia bunilizi ya fasihi simulizi iliyojengwa katika mwingiliano matini wa Biblia na fasihi simulizi. Agiso (2017) anapendekeza kuwa Biblia inaweza kutumiwa kama rejea ya maumbo ya fasihi simulizi ili wasomi wengi waweze kuisoma kama kitabu cha fasihi simulizi. Huenda mapendekezo haya yanaweza kusadifu kile tunachokiona katika kazi hii ambamo mtunzi ameweza kutumia mtindo wa kuchanganya kisa cha kubuni ili aweze kufundisha masomo yahusuyo elimu-Uungu. Ni vyema tukafahamu kuwa udhaifu wa mhusika Tupatupa unaimarishwa na shauku ya tamaa ya kuona.

Neno “kuona” limetumiwa na msimuliaji kuonesha udhaifu wa tamaa ya macho ambayo kulingana na teolojia ya Kikristo ni kiini cha maanguko ya wanadamu wengi. Uchanganyaji huu wa fasihi simulizi na ufahamu wa Biblia unaifanya kazi hii itengeneze upekee wa kimtindo. Wanjala (2015) anaona kuwa hakuna fasihi yoyote inayoweza kukamilika bila kuchanganyikana na kazi zingine za fasihi ambamo mipaka ya kitanzu huvurugwa na kufanya kazi mpya iibuke. Katika wimbo huu, msimuliaji baadaye anahama kutoka katika uimbaji na kutumia mtindo wa mazungumzo katika wimbo kama tunavyoweza kuona katika matini ifuatayo:

> Mtoto mzuri, malkia, malkia mrembo kama wewe unatembea chini, mimi nikikuoa nitakununulia ndege uifanye kama daladala itakuwa inakupeleka Ubungo *to* Kariakoo wakati mwimgine Masaki. Nitaifanya dunia iwe kijiji kidogo kwako.

Uteuzi wa maneno katika matini hapo juu umefanywa kwa makini kiasi kwamba usomaji wa kina unaweza kubainisha sifa anuai za mhusika Tupatupa. Maneno kama “mtoto mzuri, malkia, na mrembo” yanasawili tabia ya Tupatupa ambayo imeelezwa katika utangulizi kupitia wimbo kuwa kila mhusika huyu ‘alipoona wadada alijua amepona’. Lakini pia ndani ya maneno haya yaliyonukuliwa msomaji anaweza pia kubaini tabia ya Tupatupa ya kutumia utajiri alionao kama njia ya kunasa wanawake ili aweze kujifurahisha kwa anasa. Tupatupa anadai kuwa anauwezo wa kumnunulia ndege mwanamke anayeridhia matakwa ya kufanya mapenzi naye. Hii ni kusema kuwa msimuliaji anataka hadhira yake ifahamu kuwa Tupatupa anatumia nguvu ya mali ili kununua mapenzi kutoka kwa mwanamke anayemwona kuwa ni mzuri. Aidha, maneno ya Tupatupa yanafunua mandhari anuai yaliyotumiwa na mtambaji. Kuwepo kwa

maneno kama Masaki, Ubungo na Kariakoo kunamfanya msomaji yeyote akisie kuwa tukio linalosimuliwa katika wimbo huu linafanyika katika jiji la Dar es Salaam kwani maeneo tajwa yanapatikana katika jiji hilo.

Pamoja na hayo, msimuliaji amemchora mhusika akitumia mbinu ya majigambo kueleza sifa zake bainifu ili aweze kumvuta msichana anayemtafuta. Kabuta (1997) anabainisha kuwa moja ya majigambo maarufu ni yale ya mitaani ambamo mhusika hujinadi kwa kupandisha hadhi yake ili apate kukubalika kutoka kwa jinsi ya kike. Katika matini hii, Tupatupa anadai kuwa atanunua ndege ambayo binti anayemtaka ataifanya kuwa daladala itakayokuwa ikimpeleka sehemu mbalimbali za jiji la Dar es Salaam. Ukweli huu wa mbinu ya majigambo ambayo ni ya fasihi simulizi, unabainisha kuwa fasihi simulizi inakubali mabadiliko na kuifanya iingie katika nyanja za dini kama katika nyimbo za muziki wa injili. Msimuliaji ameteua njia ya picha jongefu kuileta hadhira yake na hapa amemudu kuwa na hadhira mbili: hadhira hai iliyomo ndani ya video hiyo na hadhira tuli ihusishayo watazamaji waitazamao picha hiyo jongefu.

Mbinu hii ya majigambo inajidhihirisha pia katika mazungumzo ya Tupatupa na Shetani, ambaye ni mhusika mwingine katika wimbo huu. Kabla hatujaangalia kwa kina kuhusu majigambo haya twaweza kupitia matini ifuatayo ili kuweza kuona uhakika wa jambo hilo.

> … huko jehanamu kulivutia sana. Wakamwambia ngoja tukuletee mgeni wetu ambaye ni Shetani. Akatokea Shetani akiwa na sura nzuri. Mzee Tupatupa alibahatika kumuuliza maswali Shetani. Akamwambia, “samahani Shetani , kule duniani watu wote wanasema ati wewe una mapembe.” Shetani akacheka akasema,” mimi ni *beautiful* na ni

> *handsome*. Nikikamata mke wa mtu ni lazima asahau ndoa yake. Na nikikamata mume wa mtu ni lazima asahau familia yake". Hayo ni maneno aliyoyasema Shetani. Akamwambia Shetani, "Huko duniani wanasema wewe unaroho mbaya", Shetani akasema, "hapana ningekuwa na roho mbaya walevi wangelikuwa wanaweza kununuliana makreti ya bia? Tena mimi ningekuwa na roho mbaya machangudoa wangekuwa wanaweza ku-*share* mabwana? Nigekuwa na roho mbaya wavuta sigara wangelikuwa wanaweza kupeana vipisi barabarani? Aah mimi ni mkarimu bwana, naweza kukupa kreti la bia lakini nikakunyima kibaba cha unga, kwa kweli siku hiyo Shetani alijieleza maelezo mazuri yaliyomfurahisha Tupatupa.

Katika nukuu hapo juu, tunaona jinsi mbinu ya majigambo ilivyotamalaki. Mathalani katika kujibu swali aliloulizwa kuhusu mwonekano wake, Shetani anajibu kuwa yeye hana sura kama watu wanavyomfikiria. Hata hivyo, uteuzi wa maneno katika mazungumzo yake unaonesha aina za tamathali za semi ambazo zimetumika katika ujenzi wa majigambo ya Shetani. Baadhi ya tamathali hizo ni hizi zifuatazo:

Chuku ni usemi wenye kutia chumvi jambo linalozungumzwa (Khatibu 1986: 80). Katika wimbo huu, tamathali hii ya usemi imetumiwa kama njia ya kujieleza lakini ikibeba kejeli ndani yake. Shetani anadai kuwa yeye ni *beautiful* tena ni *handsome*. Maneno haya mawili ya lugha ya Kiingereza yanamaana zinazojenga ukinzani wa kiuana. Hornby (2017) katika kamusi ya Kiingereza anakifafanua kisawe *beautiful* kuwa humaanisha "mwanamke ama msichana anayevutia kuangalia na "*handsome* huonesha mwana mume anayevutia. Maana hizo mbili zimetumika katika majigambo kujenga sifa kwa Shetani kuhusu mbinu za usasi anapokuwa anatafuta mawindo dhidi ya wanadamu.

Kejeli ni tamathali nyingine ya semi ambayo maana ya ndani ni kinyume cha yale yasemwayo (Khatibu, 1986:85). Katika wimbo huu kejeli imetumika kuelezea ukarimu wa Shetani. Mathalani, Shetani anabainisha kuwa yeye ni mkarimu aliyetayari kutoa fedha nyingi kununua vilevi na kuwagawia marafiki zake lakini asiwe tayari kuwapa chakula watu walio na njaa. Ukarimu huo huo umeelezwa kuwamo miongoni mwa wavutaji wa sigara ambao wako tayari kutumia sigara moja bila kujali madhara ya kiafya wanayoweza kuyapata kupitia maambukizi ya magonjwa mbalimbali. Aidha msimuliaji akiwa katika sauti ya Shetani, anaeleza kuwa yeye ni mkarimu kwani machangudoa wako tayari kulala na mwanamme mmoja bila kuona wivu. Kwa hakika ukarimu huu ambao unaelezwa kuwa ni ukarimu unabeba ukinzani wa maana ya ukarimu unaokubalika kimaadili. Hii ni kusema, mbinu ya ugambi imetumia tamathali mbalimbali kueleza nduni za shetani.

Mrikaria (2010) anajadili dhima ya kejeli katika fasihi kuwa mbinu hii hutumiwa na inaendelea kutumiwa na waandishi ili kuwezesha hadhira na wasomaji wafikirie kwa undani suala linaloongelewa ili waweze kupata ujumbe ulioazimiwa waupate. Wimbo huu, kwa hivyo, umetumia mbinu za fashi simulizi kuweza kuelezea dini kwa namna rahisi inayoweza kufahamika katika jamii ambamo fasihi simulizi ni sehemu ya amali ya jamii ile.

**Uhusika, mandhari na safari katika wimbo wa Tupatupa**

Fasihi simulizi, aghalabu, hutumia madhari na wahusika kibunilizi. Wahusika hawa wanaweza kuwa wanadamu, wanyama, au maumbile mengine. Hii ni kusema kuna wahusika waliohai na wahusika waliohaishwa. Mungai (2014) akizungumzia wimbo wa Mukabwa "Kiatu kivue" anabainisha kuwa madhari inaweza kutumika katika kazi ya fasihi kuashiria jambo fulani na wahusika wanaweza kuwa ni wakimazingaombwe kama wanavyobainisha Mwamzandi na Kisurulia (2020). Katika wimbo huu, kuna mandhari mbalimbali zilizotumika. Mathalani, kuna mandhari ya duniani, Jehanamu na mbinguni. Mandhari hizi zitafafanuliwa katika aya zinazofuata zikiambatanishwa na wahusika waliotumika katika kila mandhari.

Kimsingi, wahusika katika wimbo huu wanaweza kugawanywa katika makundi makuu mawili. Kuna wawahusika waliohai. Katika kundi hili tunamwona mhusika Tupatupa. Idadi iliyobaki ya wahusika ni wale waliohuishwa ambao katika wimbo huu ni Yesu, malaika Shetani, na watu wengine kama wanawake wazuri ambao Tupatupa anawaona kule Jehanamu. Hali kadhalika madhari katika kisa hiki ni ya aina kuu tatu. Yapo madhari ya duniani katika jiji la Dar es salaam wakati wa usiku ambapo Tupatupa amelewa akiwa anatembea barabarani. Kuna mandhari ya Jehanamu ambayo wakati wake unaweza kugawanywa katika makundi mawili; Jehanamu katika kipindi cha kampeni kabla ya hukumu na Jehanamu baada ya kampeni wakati wa hukumu na madhari ya mbinguni ambako Tupatupa anapelekwa baada ya kutoka Jehanamu wakati wa kampeni kama tunavyoweza kuona katika sehemu zifuatazo:

> Basi malaika akasema kwanza tunaanza kukupeleka Jehanamu. Bwana, wakaingia Jehanamu walipofika Jehanamu, mzee Tupatupa alichokiona Jehanamu kilikuwa si cha kawaida akaona Jehanamu kuna wanawake wazuri, tangia yuko duniani mzee Tupatupa hajawahi kuona wanawake wazuri namna hiyo. Akageuka tena upande mwingine, akaona ngoma nyingi zinapigwa mara ho, mdumange, segere kucheki upande mwingine, akakuta kila aina ya kinywaji kilikuwepo. Kwa kweli siku hiyo Jehanamu kulivutia sana, kilichomfurahisha Jehananu mzee Tupatupa ni wale wadada wazuri. Walikuwa na sura nzuri na nyuso za ukarimu zilizojaa tabasamu. Wakamuuliza mzee Tupatupa, tukusaidie nini kwa sura za ukarimu zilizojaa tabasamu. Basi wakamletea pombe wakamletea kila aina ya kiburudisho alichokitaka. Siku hiyo mzee Tupatupa, huko Jehanamu kulivutia sana.

Nukuu hapo juu inaonesha mandhari ya Jehanamu wakati wa kampeni. Katika wakati huo, Jehanamu pamechorwa pakiwa pamepambwa kwa kila aina ya anasa ambazo zinamfanya Tupatupa avutiwe na mambo yanayoendelea kule. Tupatupa anaona kila hitaji la moyo wake ikiwamo wanawake wazuri, ngoma za kila namna na vinywaji mbalimbali ambavyo Tupatupa anavipenda. Ni vyema tukatambua kuwa simulizi hii inatambwa katika picha jongefu ikiwa inasawili fasihi simulizi ikilenga kutoa mafundisho yahusuyo maadili na dini. Uwepo wa taarifa zihusuzo ngoma mbalimbali zinazochezwa na baadhi ya makabila ya Tanzania kama vile *segere* na *mdumange* hubainisha maingiliano ya fasihi simulizi ya Mtanzania na dini ya Kikristo kama sehemu ya imani anuai waaminizo watanzania. Mandhari haya pia kama ilivyotangualia kuelezwa, yanaonesha Jehanamu wakati wa hukumu ambapo kipindi cha kampeni kimekamilika kama tunavyoweza kuona katika sehemu ifuatayo.

> Mimi mwenyewe mzee Tupatupa, kwa hiari yangu, nimeamua kwenda Jehanamu nikiwa na akili timamu! Basi kitabu kikajifunga. Lifti ikatokea mbele yake. Akajikuta yuko Jehanamu. Bwana we alichokikuta Jehanamu si kitu cha kawaida. Aliona Jehanamu unawaka moto mkubwa. Mzee Tupatupa akamwambia malaika, hapana nataka unilete kule ulikonileta mwanzo malaika akamwambia nilikokuleta mwanzo ndio huku. Akasema hapana. Jana kulikuwa na starehe, jana kulikuwa na wanawake wazuri. Malaika akamwambia haa kumbe hukujua? Jana ilikuwa siku ya kampeni!

Katika sehemu hii ya simulizi, tunaweza kuona mandhari ya Jehanamu baada ya kampeni. Hapa tunaona kuwa eneo lote ambalo hapo awali lilipambwa kwa kila aina ya anasa halivutii tena na kumfanya Tupatupa atamani kurudi mbinguni. Mkazo mkubwa katika mandhari haya ni namna Jehanamu ilivyopambwa kwa moto ambapo katika mandhari ya Jehanamu kabla ya kampeni moto haukuwapo. Inafaa pia kusema kuwa katika fasihi simulizi wahusika ama wawe hai au waliohaishwa hupata wakawasiliana na hapana anayehoji kuwa haya yanawezekanaje kwani sifa mojawapo ya fasihi simulizi kuonesha kuwa i hai ni pale ambapo hata viumbe walionje ya urazini wa mwanadamu wanapoweza kuwa na mawasiliano halisi. Katika sehemu hii, Shetani na malaika wanazungumza moja kwa moja na mwanadamu Tupatupa. Aina hiyo ya mandhari inajitokeza kupitia mandhari ya mbinguni wakati wa kampeni kama tunavyoweza kuona katika nukuu ifuatayo.

> Mzee Tupatupa alipofika mbinguni, kweli mbinguni kulikuwa kunavutia. Alipotazama mbele yake akaona malaika. Akaona kundi kubwa la watu. Wanaimba wanasujudu. Wanaimba wanasujudu. Alipoendelea kuangalia akaona wote wanasura moja jambo ambalo lilimkwaza sana Tupatupa kwa hiyo hakupenda mazingira

> yale, maana yeye mzee Tupatupa alijua akifika mbinguni ataona wanawake wazuri lakini haikuwa hivyo. Aliona wote wanasura moja. Alishindwa kuwatofautisha, alipoangalia upande mwingine labda aone kinywaji chochote au starehe zozote aliona kule hakuna starehe yoyote zaidi ya kuimba na kuabudu …

Katika sehemu hii ya simulizi, Tupatupa anapelekwa katika mazingira ya mbinguni wakati wa kampeni. Simulizi inabainisha kuwa anapofika mahali pale Tupatupa anaona wahusika ambao ni malaika na baadaye anakutana na mhusika mkuu mbinguni ambaye ni Yesu. Hata hivyo, Tupatupa haonekani kufurahishwa na mazingira ya mbinguni kwa sababu kuu mbili: moja hapati anasa kwani yeye ni mtu anayependa anasa; pili anaona kuwa mbinguni panachosha kwa vile karibu kila jambo limefungwa kwa kanuni. Hii inajidhihirisha kupitia sura za wahusika wanaofanana, na mfumo wa ibada unaohusisha kusifu na kusujudu kunakofanywa na wakazi wa mbinguni.

Usimulizi huu wa kifasihi, ingawa umekusudiwa kutoa mafundisho ya kidini, umechota kwa sehamu kubwa mtindo wa fasihi simulizi ya mtanzania na kuiingiza katika matumizi mengine kama dini kama inavyojibainisha katika simulizi hii. Senkoro (2006) akiziangalia kazi andishi *Lina Ubani* (P. Mhando), *Jogoo Kijijini* na *Ngao ya Jadi* (E. Hussein) na *Rosa Mistika* (E. Kezilahabi) anaona kuwa fasihi hizi andishi zimeathiriwa kwa kiwango kikubwa na fasihi simulizi. Ukweli huu pia unajibainisha katika kazi hii ya Bahati Bukuku.

Wimbo huu uliokatika picha jongefu, kwa sehemu kubwa ingawa umekusudiwa kuwa wa kuinjilisha, umetawaliwa na mandhari, wahusika na motifu ya safari na mawasiliano ya wahusika. Method (2020) anabainisha

kuwa fasihi haiwezi kubaki bila kupokea mabadiliko ili ikidhi matakwa ya jamii kisiasa kiuchumi, kiutamaduni na kijamii. Lakini pia uhifadhi wa wimbo huu nikielelezo cha unyumbulifu wa fasihi simulizi ambayo kwa sasa inahifadhika na kuoneshwa kupitia picha jongefu. Kasiga na Luhwago (2019) wanabainisha kuwa fasihi simulizi ikioneshwa runingani hutengeneza uzuri kupitia picha jongefu zinazosaidiwa na ala za muziki na mapigo ya kimuziki katika utambaji wa hadithi. Kwa hakika walichobaini watafiti hawa kinaweza kuonekana katika kazi hii ya Bahati Bukuku.

Motifu ya safari ni mbinu nyingine ya fasihi simulizi ambayo inajibainisha katika wimbo huu. Safari ya kwanza ya Tupatupa inaanzia anapopata ajali kama tulivyoona katika usuli wa kisa hiki. Mara baada ya ajali hiyo, Tupatupa anapelekwa Jehanamu. Safari ya pili ni ile inayomfikisha mbinguni na safari ya mwisho ni pale anaporudishwa tena Jehanamu. Uwepo wa safari hizi unaifanya simulizi hii itengeneze motifu. Kwa hakika dhana hii ya safari ni dhana ya fasihi simulizi na fasihi andishi yenye kuathiriwa na fasihi simulizi. Vitabu viwili vya Shaabani Robert; *Kusadikika* na *Adili na Nduguze* vinabeba dhana ya motifu ya safari ambamo wahusika hukutana na maajabu. Sesoo (2020) anabaini kuwa motifu ya safari ya msako hubeba falsafa maalumu yenye kuakisi maisha ya Waafrika kama imani zao, dini, uganga na uchawi na mambo kadha wa kadha. Wimbo huu kama zilivyo kazi nyingi za fasihi simulizi umetawaliwa pia na kanuni ya motifu. Utumizi huu unaufanya wimbo huu ubaki na sifa zilezile za fasihi simulizi.

Ufasihi simulizi katika wimbo huu unaweza kutazamwa kupitia urefu wa wimbo huu. Ingawaje kwa hakika tunaweza kuuita wimbo, sehemu kidogo

mno katika wimbo huu ambapo msimulizi anaimba. Kwa sehemu kubwa utambaji umetamalaki na kuufanya wimbo huu kuwa mrefu unaochukua takribani dakika kumi na nne kama zilivyo kazi mbalimbali za fasihi simulizi. Mathalani, ziko ngoma nyingi za makabila ya Tanzania ambazo huhusisha uimbaji wenye urefu toshelevu wa wimbo wakati wa utendaji. Budebah na Bakize (2017) wanaona kuwa nyimbo za ngoma ya wigashe ambazo huimbwa na kabila la Wasukuma wa Tanzania ni ndefu mno. Uimbaji wake ambao huhusisha mkarara na maneno yatamkwayo na manju hufanya nyimbo hizi ziweze kuimbwa kwa takribani dakika thelathini hadi mia na themanini. Mbinu kama hii ndio pia imetumiwa na Bukuku katika wimbo wake kama tulivyokwisha kuona.

**Dhima ya mtambaji katika wimbo wa Tupatupa**

Safari ya mwisho anayoifanya Tupatupa inamhamisha kutoka mbinguni kwenda Jehanamu na kuifanya simulizi hii ndefu ifikie kilele chake. Yafaa tufahamu kuwa katika matini ambamo kisa kinachohusu safari ya mwisho, mtambaji anakamilisha makusudi yake kwa kutoa mafunzo aliyokusudia kwa hadhira yake kuyapata. Kabla ya kujadili kwa kina ni vyema tukaiangalia matini yenyewe kama isemavyo katika sehemu ifuatayo:

> Mimi mwenyewe mzee Tupatupa, kwa hiari yangu, nimeamua kwenda Jehanamu nikiwa na akili timamu. Basi kitabu kikajifunga. Lifti ikatokea mbele yake akajikuta yuko Jehanamu bwana we alichokikuta Jehanamu si kitu cha kawaida. Aliona Jehanamu unawaka moto mkubwa. Mzee Tupatupa akamwambia malaika, hapana nataka unilete kule ulikonileta mwanzo. Malaika akamwambia nilikokuleta mwanzo ndiyo huku, Akasema. Hapana jana kulikuwa na starehe. Jana kulikuwa na wanawake wazuri. Malaika akamwambia haa kumbe hukujua. Jana ilikuwa siku ya

> kampeni ndugu yangu, yule mtu akakasirika akasema bwana
> basi mimi sitaki huku Jehanamu nipeleke mbinguni …

Sehemu hii ya mwisho katika wimbo huu inadhihirisha kuwa kisa hiki ni cha kubuni ambacho kimekusudiwa kutoa mafunzo na maonyo yahusuyo masuala ya dini. Kama tunavyoweza kuona katika matini hiyo, Tupatupa arudipo Jehanamu, anapokelewa na Shetani kulingana na msimuliaji, akiwa na mapembe halisi. Kwa hakika msomaji yeyote makini aweza kuona shaka katika uhakika wa kisa hiki. Mathalani, Shetani anaonekana akiwa anazungumza kutoka kwenye moto. Akiwa anadondosha damu za watu. Jambo hili kwa hakika linakinzana na maandiko na teolojia ya Kikristo kwani Shetani hawezi kuwa na mamlaka dhidi ya moto wa Jehanamu kwani moto huo umeandaliwa kumwangamiza yeye pia. Sehemu ya matini ifuatayo inabainisha wazi makusudi ya msimuliaji wa kisa hiki.

> Ungejua ndugu yangu wewe unayenisikiliza kipindi hiki ni kipindi cha kampeni wagombea ni Mungu na Shetani, Hatuwezi sasa kukuuliza wewe unamuwakilisha mgombea gani. Matendo yako yanamwakilisha mgombea wako.

Msimuliaji anaweka wazi kuwa wakati huu ni wakati wa Kampeni na wagombea ni Mungu na Shetani. Kisha anabainisha kuwa tathimini ya kila mtu iko katika matendo ambayo kwa hakika hueleza upande alimo mhusika. Huenda funzo hili la mwandishi limetwaliwa kutoka maandiko matakatifu "Mtawatambua kwa matunda yao (Mathayo 7:20). Hatimaye msimuliaji ametoka katika mazungumzo na kuhamia katika uimbaji kama njia ya ukaziaji wa maana ya kile kilichosemwa kwa maneno kama tunavyoweza kuona katika mkarara wa wimbo huu.

> Ukimuona kaka anawinda wanafunzi,
> Jua ni Shetani anafanya kampeni.

Ukimuona dada anafanya ukahaba
Jua ni Shetani yuko kwenye kampeni,
Ukimuona muhubiri anamuhubiri Yesu
Jua ndiye Mungu yuko kwenye kampeni,
Ukimuona muombaji anafanya maombi
Jua Bwana Yesu yuko kwenye kampeni
Ukimuona mtu anafanya mambo mema
Jua Bwana Mungu yuko kwenye kampeni.
Ukimuona mtu anafanya mabaya
Jua ni Shetani anafanya kampeni.

Katika sehemu ya wimbo huu, mwimbaji anaorodhesha vielelezo kadhaa vya kampeni. Matendo haya yanaweza kuwekwa katika makundi mawili yaani matendo mema na matendo mabaya. Matendo yote mema ni kampeni inayofanywa upande wa Mungu na matendo yote maovu ni matendo ya kampeni iliyo upande wa Shetani. Kwa hakika kwa maelezo ya mwimbaji yanaashiria kuwa kampeni hii inamhusu kila mtu kama mwandishi asemavyo:

Kumbe hivi leo niko kwenye kampeni,
Mungu na Shetani wanafanya kampeni,
Kumbe hivi leo niko kwenye kampeni
Mungu na Shetani wanafanya kampeni.

**Hitimisho**

Wimbo huu, kama tulivyoona, umetawaliwa sana na mbinu za fasihi simulizi. Katika picha jongefu ambamo wimbo huu umehifadhiwa, msimuliaji amejivika jukumu la fanani. Picha hii ikitazamwa huonesha hadhira ambayo msimuliaji kaikusanya na kuanza kuisimulia. Ingawa kwa hakika utungo huu umekusudiwa kuwa wimbo, ni kwa kiasi kidogo tu ambamo wimbo huu unaimbwa na mwimbaji ni mmoja ambaye pia ni msimuliaji wa kisa. Hii inaufanya wimbo huu kuwa fasihi simulizi na, kwa kiasi kikubwa, unaonesha jinsi mbinu anuai za fasihi simulizi zinavyoathiri

nyanja nyingi na kujikuta ikiingia katika ujaribizi katika masuala ya dini kupitia picha jongefu. Msimuliaji pia ameweza kutumia mbinu za kauli mbalimbali za usimulizi. Katika wimbo huu, umaizi kama mbinu ya usimuliaji umetawala kwa kiasi kikubwa. Msimuliaji anaonesha kujua yaliyoko mbinguni na yaliyoko duniani. Aidha, msimuliaji anaonekana kujua hata mawazo ya wahusika waliomo katika kisa hiki. Ni vyema tukafahamu kuwa wimbo huu ni kisa mafunzo kilichofumwa katika umbo la sitiari. Mandhari na wahusika wote wanawakilisha dhana mafunzo iliyokusudiwa kuwafahamisha watu kuwa maisha ya mwanadamu yanahitaji maandalizi ambayo huamua hatima ya mtu huyo. Wimbo huu unaonesha kuwa fasihi simulizi ya Kiswahili inajigeuza na kupokea mabadiliko na kuifanya ikidhi matakwa ya jamii katika kipindi tulichonacho. Ni wimbo ambao pia unaonesha nguvu ya fasihi kujibadilisha ili kujitengenezea uhuluti kulingana na wakati na mazingira.

**Marejeleo**

Agiso, Y.O. (2017). Mwingiliano wa Matini wa Maumbo ya Fasihi Simulizi ya Kiafrika na Matini Teule za Biblia. *Tasnifu ya Uzamivu* Chuo Kikuu cha Maseno.

Barry, P. (2002). *Structuralism: Beginning Theory: An Introduction to Literary and Cultural Theory*. Manchester: Manchester University Press.

Budebah, C. & Bakize L. (2017). Mbinu za Utunzi wa Nyimbo za Ngoma za Wigashe". *Kioo cha Lugha*, 12 (1), 87 - 99.

Catman, S. (1967). Literary Style- *A symposium*, New York.

Hilary, P. (1973). Meaning and Reference. *Journal of Philosophy Department of Linguistics*. Stanford 19 (70), 699 - 711.

Hornby, A.S. (2017). *Advanced Learners Dictionary*. Oxford: OUP.

Kabuta, N. (1997). Isimu-Ushairi: Muundo wa Majigambo. *Nordic Journal of African Studies,* 6 (1), 36 - 60.

Khatibu, S. (1986). Tamathali za Semi za Kiswahili. *Mulika*, 18 (1), 76 - 91.

Kasiga, G. & Luhwago, N. (2019). Filamu ya Kiswahili: Fasihi Simulizi iliyostawi. Eldoret: Moi University Open Access Repostory.

Leach, G. & Short, M. (1981). *Style in Fiction. An Introduction to English Fictional Prose*. London: Longman.

Method, S. (2020). Hali ya Fasihi Simulizi ya Kiswahili katika Jamii ya Sasa na Mustakabali wake. *Kioo cha Lugha,* 18 (1), 189 - 207.

Mulokozi, M.M. (1996). *Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Mutembei, A.K. (2006). Nadharia ya Fasihi Simulizi na Maendeleo katika Sayansi na Teknolojia. *Mulika*, 27 (1), 1 - 17.

Mrikaria, S. (2010). Kejeli na Fasihi ya Kiswahili Tanzania. *Swahili Forum,* 17 (1), 104 - 125.

Mungai, M. (2014). Fani katika Nyimbo za Anastacia Mukabwa, (Tasinifu ya Uzamili, haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Nairobi.

Mwamzandi, I., Kenduiywa, A., & Kisurulia, S. (2020). Vipengele vya Uwasilishaji wa Wahusika wa Kimazingaombwe na Uhusika: Mifano kutoka Gehena na Babu Alipofufuka. *Jarida la Afrika Mashariki la Masomo ya Kiswahili,* 2 (1), 1 - 7.

Robert, S. (2010). *Adili na Nduguze*. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota.

Robert, S. (1991). *Kusadikika*. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota.

Senkoro, F. (2006). Fasihi ya Kiswahili Majaribio: Makutano ya Fasihi Simulizi. *Kioo cha Lugha,* 4 (1), 22 - 38.

Simpson, P. (2004). *Stylistics.A Resource Book for Students*. London: Routledge.

Sosoo, F. (2020). Ushujaa katika Motifu ya Safari ya Msako na Utamaduni na Falsafa ya Kiafrika. *Kioo cha Lugha,* 18(1), 152-171

Wanjala, F.S. (2011). *Kitovu cha Fasihi Simulizi kwa Shule na Ndaki*. Mwanza: Serengeti Bookshop.

Wanjala, F.S. (2015). Nadharia ya Mwingiliano Tanzu katika Uhakiki wa Fasihi Simulizi. (Tasinifu ya Uzamivu, haijachapishwa), Chuo Kikuu Kenyatta.